

# **TANGAZO**

## **HALMASHAURI YA WILAYA YA RUNGWE**

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe anawatangazia Wafanyabiashara wote wa Soko Kuu, Soko la Machinga (Stendi ya vumbi) na stendi kuu Tukuyu kutuma maombi kwa ajili ya ujenzi wa vibanda vya biashara katika maeneo yafuatayo:-

1. Eneo la Soko Kuu
2. Eneo la Stendi ya Vumbi
3. Eneo la ukumbi wa maendeleo (Garden)

### **MASHARTI NA VIGEZO VYA MAOMBI**

#### **1. UJENZI WA VIBANDA ENEO LA SOKO KUU TUKUYU NA STENDI KUU**

- a) Awe na mkataba na Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe
- b) Awe na leseni ya biashara na TIN
- c) Awe mfanyabiashara wa eneo husika
- d) Awe mlipaji wa kodi ya kibanda; malipo yawe yamefanyika hadi kufikia mwezi Disemba 2017 na asiwe na deni lolote la kodi ya kibanda

#### **2. UJENZI WA VIBANDA ENEO LA SOKO KUU TUKUYU (KWA WAFANYABIASHARA WANAOAMILIKI VIZIMBA ENEO LA SOKO KUU)**

- a) Awe mfanyabiashara wa eneo la soko
- b) Awe analipa ushuru wa Halmashauri na historia yake ya ulipaji ionekane ushuru umelipwa hadi kufikia mwezi Disemba, 2017

#### **3. UJENZI WA VIBANDA ENEO LA STENDI YA VUMBI**

- a) Awe na leseni ya biashara na TIN
- b) Mlipaji wa Kodi ya Kibanda. Malipo yawe yamefanyika hadi kufikia mwezi Disemba 2017 na asiwe na deni lolote la kodi ya kibanda

**4. UJENZI WA VIBANDA ENEO LA STENDI YA VUMBI (KWA MACHINGA WA STENDI YA VUMBI WANAOTAKA KUJENGA VIBANDA ENEO LA STENDI YA VUMBI)**

- a) Awe mfanyabiashara wa eneo la stendi ya vumbi (Machinga)
- b) Awe analipa ushuru wa Halmashauri na historia yake ya ulipaji ionekane ushuru umelipwa hadi kufikia mwezi Disemba, 2017
- c) Awe hajawahi kutelekeza meza/kukodisha kwa mtu mwingine

**5. UJENZI WA VIBANDA ENEO LA GARDEN**

- a) Awe mfanyabiashara wa eneo la stendi ya vumbi
- b) Awe analipa ushuru wa Halmashauri na historia yake ya ulipaji ionekane ushuru umelipwa hadi kufikia mwezi Disemba, 2017
- c) Awe hajawahi kutelekeza meza

**MASHARTI YA JUMLA YA MWOMBAJI:**

1. Awe na uwezo wa kujenga kibanda ndani ya muda uliopangwa
2. Awe tayari kufuata maelekezo na taratibu zinazotolewa na Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe
3. Maombi yote yatumwe kwa njia ya barua kwa Mkurugenzi Mtendaji Wilaya ya Rungwe kwa anwani ya S.L.P 148 Tukuyu. Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe **10.1.2018**



**Loema I. Peter**

**MKURUGENZI MTENDAJI (W)**

**RUNGWE**